# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KIBAIGWA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Mkuu wa Shule +255 768- 952222**

**+255 768-806393**

**Makamu Mkuu wa Shule +255 629-293554**

**+255 735-000091**

**Matron +255 766-816468 / 0717060636**

**Shule ya Secondari ya wasichana Kibaigwa**

**S.L.P 05**


**Tarehe ......................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KIBAIGWA HALMASHAURI YA KONGWA, MKOA WA DODOMA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari ya wasichana kibaigwa ipo umbali wa Kilometa **37** kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya kongwa. Shule inapatikana ndani ya Mamlaka ya Mji wa Kibaigwa, umbali wa kilometa **3** kutoka stendi kuu ya madasi ya kibaigwa (dodoma-dar es salaam/ dodoma morogoro/ morogoro-dodoma). Usafiri wa pikipiki au bajaji kutoka stendi ya mabasi kibaigwa kuja shuleni ni **TZS. 2,000/=** unapatikana katika kituo cha mabasi kibaigwa.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **14/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

i. Sare ya shule hii ni **sketi rangi ya kijivu, kitambaa kizito, mshono wa marinda kama yanavyoonekana kwenye picha.**

**NB: 1.** Ili kuepuka kutochanganya rangi ya sketi pamoja na mshono **UNASHAURIWA** mwanafunzi ashone sketi hiyo hapahapa shuleni kwa bei ya **TZS. 20,000/= KWA SKETI MOJA.** Aidha fedha hiyo aje nayo taslimu, atakaporipoti, atalipia na kupewa stakabadhi kisha kufanya vipimo ili kushonewa sketi yenye muonekano unaotakiwa.

**NB: 2.** Kwa wanafunzi wa kiislamu watavaa mashati kama ya wanafunzi wengine, sketi kama wanafunzi wengine na **HIJABU NYEUPE** inayofunika kifua na isivuke kiuno.

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.

iii. Sare ya Michezo ni track suit, rangi ya blue, kubwa, nzito isiyoonyesha maumbile ya mwili(isiyobana), bukta rangi nyeusi isiyobana, T-shirt nyeupe na raba za rangi nyeusi.


iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili (2) nyeupe ziwe ndefu.

vi. Sweta la rangi ya kijivu lenye umbo la ”V” kifuani.

vii. Nguo za kushindia ni gauni la marinda manane,mikono mifupi,shingo ya duara,urefu wa cm 30 kutoka usawa wa magoti( rangi ni “Draft” ya blue na nyeupe. NB:Unashauriwa kutumia kitambaa **KIZITO** au kuweka “**LINING**” wakati wa kuishona.

viii. Tai ni fupi yenye rangi ya kijivu inayofanana na rangi ya sketi ambapo itatolewa pamoja na sketi kwa gharama ileile iliyotajwa kwa sjeti moja.



**NB:Muonekano wa mbele na nyuma unafanana na urefu wa sketi unatakiwa uwe chini ya magoti kwa cm 15.**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Vifaa vya darasani. Madaftari makubwa **14 (Quire 3 au 4**), Daftari ndogo (Msomi) a kutosha kuokana na tahasusi yake, rula, kalamu za kutosha, penseli na ufutio, begi zuri na imara kwaajiri ya kubebea daftarina mathematical set moja.

ii. **Ream ya karatasi nyeupe A4** Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Mwanafunzi anatakiwa kuja na Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma **CBG.**

v. Koti jeupe la maabara lenye muonekano mzuri kwa wanafunzi wanaosoma **CBG.**

vi. Scientific Calculator kwa wanafunzi wote wanaosoma Geography;

vii. Mwanafunzi anapaswa kuja na godoro **2.5 x 6.**

viii. Mashuka Jozi **2** ya **rangi ya pink,** blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 chenye ukubwa wa **futi 3 au 4 square** ambayo ni **rangi ya pink,** taulo **rangi ya pink** na jozi moja ya kanga au kitenge. (*Nguo nyingine yeyote ambayo haijatajwa kuwa ni sare ya shule* ***HAIRUHUSIWI KABISA****);*

ix. Nguo za ndani za kutosha;

x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na kidumu kimoja chenye ujazo wa lita tano kwaajiri ya kutunzia maji ya kunywa.

**VIFAA VYA USAFI**

Kila mwanafunzi anapaswa kuja na kifaa cha usafi kulingana na maelekezo ya fomu hii kulingana na tahasusi yake kama ifuatavyo,

1. **HGE na CBG.** Wanafunzi waliochaguliwa kwenye tahasusi hii wanatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo,
   I. Jembe jipya 1 lenye mpini
   II. Kwanja moja (1) imara
   III. Mfagio wa nje mmoja (1) ( **chelewa yenye mpini**)
   IV. Mooper moja (1). (**dekio**)
2. **EGM na HGK.** Wanafunzi waliochaguliwa kwenye tahasusi hii wanapaswa kuja na vifaa vifuatavyo,
   I. Reki yenye mpini wa chuma moja (1).
   II. Kwanja moja (1) imara.
   III. Mfagio wa ndani mmoja (1) wenye mpini wake. (**soft broom**)
   IV. Hard broom moja (1) **yenye mpini**.

**2.3 Michango mbalimbali**

Jumla ya michango ya shule ni TZS. 80,000/= na inapaswa kulipwa kwa njia ya benki kupitia akaunti namba hii hapa; **50310025414 NMB, KIBAIGWA GIRLS SECONDARY SCHOOL CAPITATION.**

**a) Mchanganuo wa michango ya shule**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Kumbuka kuandika jina lako kwenye risiti ya malipo na utakabidhi wakati unaripoti shuleni.

## Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo. (utoro).
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa, usagaji;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kutofuata na kuzingatia ratiba ya shule kwa makusudi.
xix. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu cha mkuu wa shule.

xx. Kukutwa unapika ndani ya bweni au kwenye jiko la shule.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (***Medical Examination Form***) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu endapo kuna tatizo usisite kuwasiliana nasi kupitia namba zilizowekwa kwenye fomu hii.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KIBAIGWA**

.................................................................

**MWL. JEMA EMILYO KIHWELO**

**Mobile phone: 0768 952222/ 0768 806393**

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMISTRESS
P.O.BOX 05
KIBAIGWA
KIBAIGWA GIRLS SEC. SCHOOL

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0768- 952222/0768 806393**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0629 293554/0735000091**

# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KIBAIGWA

# FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi (majina kamili) ……………………………………………………. Nimekubali kuingia kidato cha ……… katika shule ya wasichana Kibaigwa kuanzia tarehe …… hadi nitakapo maliza kidato cha …………..
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za shule na kushiriki katika shughuri zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa …………… Kijiji………….. Tarafa ……….wilaya………… shule unakotoka ………….. namba ya mtihani ……………………
4. Kituo cha gari (bus) Gari moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako ……………..

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. Mimi (majina kamili) ………………………………………………. Nimekubali mtoto wangu asome katika shule ya wasichana Kibaigwa kuanzia kidato cha tano hadi atkapomaliza kidato cha sita nakubaliana na sheria na kanuni za shule
2. Jina la mama ……………………………………………………..
3. Jina la baba ……………………………………………………
4. Anuani ya mzazi/mlezi na namba ya simu …………………………
5. Mtaa/mji ………………….. Kata………… Wilaya ……………………. Mkoa……………………………………
6. Wafuatao ni ndugu zake ninaowatambua wanaishi hapa Dodoma na wanaweza kumsaidia mwanangu wakati wa dharura.

i) Jina kamili…………………………………………………….. mahusiano………….. anakoishi ………………Namba ya simu ………………

ii) Jina kamili…………………………………………………….. mahusiano………….. anakoishi ………………Namba ya simu ……………

iii) Jina kamili…………………….. mahusiano………….. anakoishi …………………………………Namba ya simu ……………………………

iv) Jina kamili…………………………….. mahusiano………….. anakoishi …………………………………Namba ya simu …………………………….

7. Dini ya mtoto ……………………………………………………………………….
8. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa anuani;- …………………………………………………………………………………………… ………………………………………………………………………………

Saini ya mzazi/mlezi ………… Tarehe ……………………………….

# Medical Examination form

**To be completed by a Medical officer**

………………………………………………………………………… (Insert name of the government medical Institution)

Name of student …………………………………………….. Form………… Year

Age …………………………….. Sex ………………………..

Blood count …………………………………………………………

Stool ………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………..

T.B Test ……………………………………………………………..

Eyes ……………………………………………………………

Ears ……………………………………………….……………

Chest ……………………………………………………………

Spleen …………………………………………..…………………

Abdomen ……………………………………….…………………

Teeth ……………………………………………..………………

Addition information ;- (Pregnancy, Physical defects, Infection, Psychological disorder, Cronic or diseases …………………………………………………

I certify that above pupils is fit to continue studies in secondary

Name of medical officer ………………….. Signature ……………………

Designation ……………………………………………………………….

Station and Official stamp ……………. Date ………………………………

**SHARTI mtoto apimwe kikamilifu kabla ya Daktari kujaza fomu hii, ikigunduliwa kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, Wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa**.